

# BWANA NDIYE MCHUNGAJI WANGU

Zab. 23: 1-6 (K) 1

Fr. Anga Anselim

Kipalapala Senior Seminary-2023

$\text{♩} = 70$

Soprano/Alto

Tenor/Bass

Bwa na ndi ye mchu nga ji wa ngu, si ta pu ngu ki wa na ki tu.

S/A

1. Bwana ndiye mchungaji wangu,  
Sitapungukiwa **na kitu**;  
Katika malisho ya majani mabichi hunilaza,  
Kando ya maji ya utulivu **huniongoza**.

2. Hunihuishanafsi yangu,  
Na kuniongoza/ katika njia za haki/  
kwa ajili ya **jina lake**.  
Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti;  
Sitaogopa mabaya/ kwa maana wewe upo pamoja nami/  
Gongo lako na fimbo yako **vya nifariji**.

3. Waandaa meza mbele yangu/  
Machoni pa watesi **wangu**.  
Umenipaka mafuta kichwani pangu/  
Na kikombe changu **kinafurika**.

4. Hakika wema na fadhili zitanifuata/  
Siku zote za maisha **yangu**  
Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana **milele**.